AFRICAN UNION

الاتحاد الأفريقي

UMOJA WA AFRIKA

UNION AFRICAINE

UNIÃO AFRICANA

**AFRICAN COURT ON HUMAN AND PEOPLES' RIGHTS**
**COUR AFRICAINE DES DROITS DE L'HOMME ET DES PEUPLES**
**MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADMU NA WATU**
S.L.P 6274 Arusha, Tanzania Simu: +255 27 2970 430 /431/432/433/434

Tovuti: www.african-court.org Barua pepe. registrar@african-court.org

AFCHPR/PTS/2022/107
Tarehe: 20 Aprili 2022

# WITO WA KUTANGAZA NIA
# KUANZISHA KANZIDATA YA WATAALAM BINAFSI WALIOKIDHI VIGEZO

## WAKALIMANI

## I. USULI

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ilianzishwa na Itifaki ya mwaka 1998 ya Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binadamu ili kuanzisha Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Hitifaki). Hitifaki ilianza kutumika tarehe 25 Januari 2004, ikiandaa njia ya uanzishwaji wa Mahakama ya Haki za Binadamu na Watu AFCtHPR. Ni chombo cha kwanza cha sheria barani Afrika chenye jukumu la kulinda haki za binadamu na watu. Mamlaka ya msingi ya Mahakama hii ni kukamilisha mamlaka ya kiulinzi ya Kamisheni ya Haki za Binadamu na Watu iliyopo Banjul (Kamisheni). Makao makuu ya Mahakama iko Arusha, Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

## II. NIA NA MADHUMUNI

Ili kuweka sawa kanzi data yake, Mahakama inatangaza na fasi kwa wakalimani wa kujitegemea wenye sifa zinazostahili katika lugha ya Kiarabu, Kiingereza, Kifaransa, Kireno, Kihispania na Kiswahili ambao ni raia wa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika.

## III. NAFASI

Wakalimani wa kujitegmea wanaalikwa kuonesha nia kwa kutoa huduma kwa njia ya mtandao na ana kwa ana (kwa mfano, wakati wa vikao na mikutano mingineyo ya Mahakama). Watapewa mikataba ya kutoa huduma za ukalimani kwenye mikutano iliyoandaliwa na itakayoandaliwa na ofisi ya Msajili wa Makama.

## IV. SHUGHULI KUU

Wakalimani wa kujitegemea watatoa huduma za ukalimani sawia (wa moja kwa moja) au fuatizi zenye ubora, kama itakavohitajika, wakati wa vikao na mikutano iliyoandaliwa na Mahakama kwa kutumia teknolojia husika.

## V. VYETI VINAVYOHITAJIKA

- Shahada ya Uzamili kwenye ukalimani, Sayansi ya Binadamu na Lugha au Nyanja yoyote inayofanana na hizo, na kuwa na uzoefu ambao siyo chini ya mika mitano (5) kama mkalimani, ikiwezekana kwenye shirika la kimataifa. Sifa ya juu katika nyanja tajwa zitaongeza manufaa.

Au

- Shahada kwenye Ukalimani, Sayansi ya Binadamu na Lugha au Nyanja yoyote inayofanana na hizo na kuwa na uzoefu ambao siyo chini ya miaka saba (7) kama mkalimani, ikiwezekana kwenye shirika la kimataifa.
- Uzoefu katika shughuli za Mahakama na Mahakama zingine za ndani na za kimataifa, utaongeza manufaa ya ziada
- Msingi wa kisheria au ujuzi wa msamiati wa kisheria utaongeza manufaa.

## VI. UJUZI UNAOHITAJIKA

- Uwezo wa kufanya kazi ana kwa ana (ofisini) au kwa njia ya mtandao.
- Uwezo wa kufanya kazi kwa shinikizo baada ya kupata taarifa ya muda mfupi.

## VII. MUDA WA KUTOA HUDUMA ZA KITALAAM

Wombaji wataokidhi vigezo watapewa mkataba wa miaka mitatu (3) ambao kutakuwa na uwezekano wa kurefushwa (kuongezewa muda).

## VIII. MALIPO

- Ukalimani kwa njia ya mtandao (vikao na mikutano):

Dola za Kimarekani 468 kwa siku.

- Ukalimani wa ana kwa ana (vikao na mikutano mingine)

Dola za Kimarekani 468 kwa siku + na pesa za kuikimu kulingana na mahali ambapo shughuli zinafanyika.

Mahakama itagharamia safari kwa wale wenye mikataba ya ukalimani wa ana kwa ana kwa kuzingatia sera za Umoja wa Afrika zinazohusu safari (Tiketi moja ya ndege kwenda na kurudi ya daraja la kiuchumi).

Malipo yote yatafanyika kwa kuzingatia kanuni na taratibu za Umoja wa Afrika.

Mahakama inayo haki ya kubadilisha kwa muda wowote viwango tajwa hapo juu.

## IX. VIGEZO VYA TATHMINI

- Historia ya kielimu (30%)
- Uzoefu wa kitaaluma (45%)
- mchepuo wa lugha (15%)
- Uwezo wa kukalimani kama mtu wa kati (10%)

## X. NYARAKA ZA KUAMBATISHA NA MAOMBI

Maombi yanapaswa kujumuisha:

- Fomu ya mwombaji iliyojazwa (imeambatishwa), ikifafanua mchepuo wa lugha (kwa mfano., EN/AR: EN/FR; EN/PT; EN/SW, N.K.)[1]
- Nakala za vyeti, uthibitisho, n.k.
- Nyaraka saidizi na maelezo ya kina kuhusu uzoefu wa kazi (mikataba, viambo vya barua pepe zinazohusiana na mikataba ya ukalimani (moja kwa kila mwaka wa uzoefu, n.k.)

Maombi yanayoonesha sifa za kitaaluma au uzoefu wa kazi usioendana na nakala za vyeti, mikataba na / au viwambo au agizo la ununuzi wa mikataba hiyo haitazingatiwa.

## XI. UWASILISHAJI WA MAOMBI

Maombi yote lazima yawe na maneno yafuatayo **"TANGAZO LA MAOMBI ILI KUINGIZA WATAALAM WA UKALIMANI KWENYE KANZIDATA YA MAHAKAMA YA AFRIKA**".

---

[1] Kiingereza/Kiarabu; Kiingereza/Kifaransa;Kiingereza/Kireno; Kiingereza/Kiswahili, n.k.

Maombi yanapaswa kutumwa kwa njia ya barua pepe kupitia: tender@african-court.org (Ukubwa wa juu wa viambatisho ni MB 25. Ikiwa ukubwa wa viambatisho unazidi MB 25, tafadhali tuma zote kwenye barua pepe tofauti).

Au

Kwa njia ya posta kupitia anwani ifuatayo:

Msajili,

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

S.L.P 6274

Arusha, Tanzania

Au

Kuwasilisha moja kwa moja Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, TANAPA, Mwalimu Julius Nyerere Conservatory Centre, Phase II, Dodoma Road. Arusha, Tanzania.

## XII. TAREHE YA MWISHO YA KUWASILISHA MAOMBI

Tarehe na muda wa mwisho wa kupokea maombi ni 20 Mei 2022 saa 11:00 jioni (GMT+3).

Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na sisi kupitia barua pepe ifuatayo: procurement@african-court.org

**Dr Robert W. Eno**

**Msajili wa Mahakama**

AFRICAN COURT ON HUMAN AND PEOPLES' RIGHTS
The Registrar
LE GREFFIER
ARUSHA TANZANIA
COUR AFRICAINE DES DROITS DE L'HOMME ET DES PEUPLES